



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS



TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI  
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

**MKOA WA KILIMANJARO**

Simu : 27-29 74369

Fax : 27- 29 74368

Email: [ded@haidc.go.tz](mailto:ded@haidc.go.tz)

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya Hai,  
3BR-TTCL-Kanisani,  
25382. Bomang'ombe,  
S.L.P. 27,  
**HAI KILIMANJARO**

Kumb.Na.LG/B.20/2/133

Tarehe: 24/05/2022

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai amepokea kibali cha kutekeleza Ikama na Bajeti kwa Ajira Mpya kwa mwaka wa fedha 2021/2022 chenye Kumb. Na. FA.97/228/01/9 cha tarehe 13 Mei, 2022 kilichotolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, hivyo anatangaza nafasi za kazi kwa wananchi wa Tanzania wenye sifa na ujuzi wa nafasi zifuatazo:-

**1 Dereva Daraja la II (nafasi 4)**

**Sifa za mwombaji:**

- Awe na elimu ya kidato cha nne (IV)
- Leseni ya Daraja E au C, ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja (1) bila kusababisha ajali.
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji wa magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambulika na Serikali.
- Waombaji wenye cheti cha majaribio ya ufundi Daraja la kwanza

**Majukumu ya kazi ya Udereva**

- i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari,
- ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi,
- iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari,
- iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari,
- vi. Kufanya usafi wa gari na
- vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake

**MSHAHARA**

- Kwa kuzingatia Ngazi ya Mshahara wa Serikali yaani TGS B kwa mwezi

## **2. Katibu Mahsusi III (nafasi 4)**

### **Sifa za mwombaji:**

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne au sita waliohudhuria mafunzo ya uhazili na kufaulu mtihani wa Hatua ya Tatu. Wawe wamefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na wawe wamepata mafunzo ya kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika program za **windows, Microsoft Office, Internet, Internet, E-mail na Publisher.**

### **Kazi na Majukumu ya Katibu Mahsusi III**

- i. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida
- ii. Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa
- iii. Kusaidia kutunza taarifa/ kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika Ofisi anamofanyia kazi, kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- iv. Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.
- v. Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao
- vi. Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa maofisa walio katika sehemu alipo na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika
- vii. Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wa kazi.

### **MSHAHARA**

- **Ngazi ya Mshahara wa Serikali ni TGS B kwa mwezi**

### **3. Mhudumu wa Jikoni/Mess Daraja la II (Nafasi 3)**

#### **Sifa za mwombaji**

Kuajiriwa wahitimu wa Kidato cha nne wenye uzoefu wa kazi kwa muda usiopungua miaka mitatu

#### **Kazi za kufanya**

- i) Kusafisha vyombo vya kupikia
- ii) Kusafisha vyombo vya kulia chakula
- iii) Kusafisha meza itumiwayo kwa kulia chakula
- iv) Kuwatayarishia wapishi/waandazi vifaa vya mapishi na mezani
- v) Kusafisha maeneo ya kulia chakula na kupikia
- vi) Kuwasaidia waandazi wa na wapishi

#### **MSHAHARA**

- **Ngazi ya Mshahara wa Serikali ni TGOS A kwa mwezi**

## MASHARTI KWA UJUMLA:

1. Mwombaji lazima awe Raia wa Tanzania.
2. Awe na Umri wa miaka 18 hadi 45.
3. Awe mwadilifu na asiwe na historia ya uhalifu
4. Waombaji waambatishe nakala za cheti cha kuzaliwa, vyeti vya kuhitimu mafunzo na vyeti vya kidato cha nne vilivyothibitishwa na wakili au mahakama
5. Testimonials, provisional results, Statement of results na hati za matokeo ya kidato cha nne na sita (Form IV na Form VI result slip) havitakubalika.
6. Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatishe uthibitisho kutoka mamlaka husika (TCU) wahakikishe vyeti vyao vimekaguliwa na kuthibitishwa na mamlaka husika.
7. Uwasilishwaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
8. Waombaji waambatishe maelezo binafsi (CV)


Mwombaji mwenye sifa anatakiwa kutuma maombi kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya Hai,  
3BR-TTCL-Kanisani,  
25382. Bomang'ombe,  
S.L.P. 27,  
**HAI KILIMANJARO**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **06/06/2022 saa tisa na nusu alasiri.**

NB:Tangazo hili linapatikana katika tovuti ya Halmashauri [www.haidc.go.tz](http://www.haidc.go.tz), tovuti ya secretarieti ya ajira [www.ajira.go.tz](http://www.ajira.go.tz) na katika mbao za matangazo za Halmashauri.

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:-**



Dionis M. Myinga  
**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
HAI  
MKURUGENZI MTENBAJI W  
HAI**

Nakala: Katibu,  
Ofisi ya Rais,  
Secretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,  
S.L.P. 2320,  
**DODOMA**



*Sensa kwa Maendeleo/Jiandae kuhesabiwa siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022*